**KANISA LA KIANGILIKANA LA KENYA**

**JIMBO LA KITALE**

**KITABU CHA MAFUNDISHO YA UWAKILI**

# WAJIBU NA JUKUMU LETU LA UWAKILI

*Kukumbatia mambo mapya Mungu anatenda*

Isaya 43:19-20

.

# DIBAJI

1.MPANGILIO WA MADA NA MAFUNZO...............................

2.UTANGULIZI.......................................................................

3.JUMA LA KWANZA:MAANA YA UWAKILI/UONGOZI...........

4.JUMA LA PILI- UMUHIMU WA WAKRISTO KUTOA....

5.JUMA LA TATU.-MSINGI WA WAKRISTO KUTOA.................

6.JUMA LA NNE-FAIDA ZA UAMINIFU KATIKA UWAKILI........

## MPANGILIO WA MADA NA VIFUNGO VYA BIBILIA

| TAREHE | MADA NA VIFUNGO VYA BIBILIA |
|---|---|
| 4/11/2018 | Mada:-maana ya uwakili.<br>Mafunzo makuu kutoka kwenye Biblia.<br>Mwanzo:-1:1 ,Ufunuo 4:11 Zaburi 24:1<br>Hagai 2:8,Matendo ya mitume 17:28 ,1<br>Wakorintho 4:7 |
| 11/11/2018 | Mada:Umuhimu wa wakristo kutoa/,,<br>Mafunzo kutoka kwenye Bibilia.<br>Matayo 6:1-4.1 Wakorintho 16:1-2<br>2Wakorintho 8:9-15 na 9:6-7 |
| 18/11/2018 | Mada:Misingi ya wakristo kunitolea Mungu .<br>Masomo kutoka kwa vifungu vya bibilia.<br>Zaburi 8.Luka 12:35-48.<br>2 Wakorintho 8:1-15.2Wakorintho 9:1-15. |
| 25/11/2018 | Mada:Faida za uaminifu katika uwakili.<br>Mafunzo kutoka kwenye bibilia.<br>Malaki 3:7-18.Zaburi 81.2Wakorintho 9:6-15.<br>Wafilipi -4:10-20. |

**UTANGULIZI.**

Kanisa la Kiangilikana Jimbo la Kitale pamoja na Kamati ya Usimamizi wanakukukaribisha kwa mafundisho ya usimamizi na msururo wa mafunzo.

Msururu hu umepangiliwa kufundishwa kwa majuma manne mtawaliwa –Jumapili nne katika Jimbo letu. Kamati yakukaribisha wewe binafsi na kanisa kwa safari ya uvumbuzi na mwito katika ukiristo ili tuwe wakili wema na waaminifu katika yote ambayo Mungu ametupa kusimamia.

Katika msururo ya mwaka huu tutaangazia mada **"Wajibu wa mkristo na uwajibikaji"** Tutaangazia mada nne kuu katika mafunzo haya kuanzia Novemba 4 hadi 25. Hii itafuatiwa na usambazaji wa kadi za kuweka agano kuanzia Novemba 18 hadi Disemba. Kila Parokia itapangilia Jumapili ya wakfu tarehe 30/12/2018 ama kabla ya hiyo tarehe.Ni Maombi yetu kwamba tutafanya kazi kwa pamoja katika safari hii kuwa waamininifu tunapoazimia kukumbatia mambo mapya na makuu ambayo Mungu karibu kuyatenda.

**SHUKRANI.**

Kamati ya uwakili yatambua kwa dhati Askofu Mkuu wa Jimbo la Kitale Daktari Emmanuel Chemengich kwa ushauri na himizo katika kutoa nakala hii. Vile vile tunashukuru Kasisi Mkuu Kosgey,Kanoni Mkuu Bi.Sarah Khisa na Kasisi Herbert Weyao kwa juhudi zao katika kukitoa kijitabu hiki. Mola abariki kila mmoja wenu.

.

**JUMA I.**

**MAANA YA UWAKILI/UONGOZI/USIMAMIZI .**

<u>Somo:</u> *Mwanzo 1:1,ufunuo 4:11,Zaburi 24:1,Hagaii 2:8,Matendo ya Mitume 17:2,1 Wakorintho 4:7.*

Wakili-ni mtu anayeongoza au anayesimamia mali ya mtu fulani au rasilimali.

Ni mchakato au hali ambayo mwanadamu amepewa wajibu na Mungu la kusimamia na kutumia kikamilifu kile ambacho Mungu wetu ametupa kwa ukarimu.

Kwa maana hii, uakili ni hali ya kusherehekea maisha yetu yote kama Imani kusimamia kwa niaba ya Bwana Mungu wetu. Wakristo wanajihusisha kwa uakili katika sehemu zifuatazo.

Fedha, mali ,talanta, vipawa,maisha ,mazingira na rasilimali zote zilizomo mkononi mwa mwanadamu.

Kwa vile jinzi tulivyo na vyote tulivyo navyo ni Imani ambayo tumepewa kwa sisi kwa ukarimu kama mawakili ni Sharti tusimamie yote kulingana na thamani kanuni na kipaumbale kwa mwenyezi Mungu.

Mambo mawili ya kimsingi kwa Mkristo wakili .

1. Kuleta watu karibu kwenye uhusiano na Mungu kupitia uzoefu wa kutoa.
2. Kupeana njia na rasilmali ya kuendeleza makusudi ya Mungu na ufalme wa Mungu duniani.

Kwa sababu hii Ron Blue atueleza maana ya uakili kama **“kutumia rasilmali tulizopewa na Mungu ili kuyafikia malengo ya Mungu”**(*Ron Blue, Kudhibiti Hela Zako uk 23*)

**Kanuni za Biblia katika uakili/uongozi/usimamizi.**

Hapa kuna kanuni sita kuu kuhusu uakili .

I. **Kanuni ya muumba**:Mungu ndiye muumba wa vitu vyote duniani na mbinguni. Mwanzo 1:1 ,Ufunuo 4:11.

.

ii. ***Kanuni ya Umiliki****:*Bwana Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote alivyoviumba Zaburi 24:1 ,Hagai 2:8.

iii. ***Kanuni ya kudhibiti/udhibiti:***Bwana Mungu anadhibiti na kusimamia vitu vyote katika himaye yake mapenzi yake ,upendo na nguvu zake.Matendo ya Mitume 17:28 Kanuni hizi zatukumbusha sisi kama binadamu kumtegemea Mungu. Kwa hivyo sharti tusiwahi fikiria kwamba twajitegemea na kumiliki vitu ijapokuwa kupewa na Mungu.

iv. ***Kanuni ya Neema /Majukumu*** :Bwana Mungu wetu ametukirimia sisi wanadamu kama wakili/walinzi wa uumbaji waki katika makusudi yake na mipango . 1Wakorintho 4:7.

v. ***Kanuni ya Uwajibikaji***:Siku moja kila mkristo atapeana hesabu ya uwajibikaji wake Luka 12:48.

vi. ***Kanuni ya kutuzwa:*** Kila mkristo sharti atapata furaha na Baraka zake katika jukumu lake la uwakili katika uumbaji wa Mungu na atatuzwa kulingana na uaminifu wake.2 Wakorintho 9:7.

Maana ya Kanuni hizi ni:

a. Mkristo Sharti awe mnyenyekevu katika kutekeleza uwakili wake.

b. Mkristo lazima awe mwaminifu na awajibike kwa Bwana wake.

c. Mkristo lazima asijiondoe katika kusimamia maswala ya ulimwengu huu kwa kuwa wao ndio wadhamini katika usimamizi wa hayo maswala pia.

**Kwa nini tunakosa kutii mwito wa Mungu kuwa mawakili wema.**

1. Mtazamo wetu potovu kuhusu fedha.

   Kwanza tunaona kuwa mali ni yetu na sio ya Mungu.

   Pili twafikiri kutoa kwetu ni kitendo cha huruma kwa kazi ya Mungu wala sio amri.
   na Si amri.

   Tatu ,twafikiri kwa kufanya huvyo twamfanyia Mungu huruma kwa kupeana kwa Kanisa lake.

2. Matumizi yetu mabaya ya fedha na mali.
   Kanuni mbili kuu zaongoza jinsi ya kutumia fedha.

   a. Jinsi tunavyopata nyingi ndivyo tunavyopata hadhi ya maisha yetu.

   b. Lazima tuwekeze fedha zote tunazopata.

Maswali ya kutafakari /kujiuliza.

1. Je,maana ya wakili katika muktadha wa dondoo hili la mafunzo,wabadilisha jinsi unavyoelewa majukumu katika maisha yako na yote sunayomiliki?

2. Je,wapuuza kanuni ipi ya uwakili s/uongozi/usimamizi mara kwa mara?
3. Je,kutafanyika nini katika maisha yako unapopuuza kauni hizi?

**JUMA LA PILI.**

**UMUHIMU WA MKRISTO KUJITOA.**

*Mafunzo Matayo 6:1-4     1 Wakorintho 16:1-2, 2 Wakorintho 8:9-15 na 9:6-7*.

Katika somo la pili,tunapeana umuhimu wa mkristo kujitoa  ili kuwajulisha au kubadilisha mtazamo wa mafunzo yetu na mazoea ya Mkristo katika uwakili. Tutatumia vifungu vifuatavyo katika Agano Jipya ili kuwajuza kuhusu umuhimu huu.Matayo 6:1-4,  1 Wakorintho 16:1-2,2 Wakorintho 8:9-15 na 2 Wakorintho  9:6-7. Kutokana na vifungu hivi vine tunabaini umuhimu  sita ufuatao wa Mkristo kutoa:-

1. **Bwana Yesu Kristo anataraji na kutazamia kila Mkristo kutoa.**
   Katika Matayo 6:2,Yesu alisema "Basi wewe utoapo"na sio "kama /ikiwa utatoa) Hi  inamaanisha kwamba Mkristo anapotoa si kwa hiari bali ni sehemu muhimu wa mwito wetu wa ukristo.Kutoa hakukuwa kwa watu wa Agano la Kale tu bali pia kwa Wakristo wa Agano Jipya.
2. **Yesu anamwita kila mkristo kutoa kwa sababu stahiki/inayofaa.**
   Bwana Yesu Kristo aliwaonya wanafunzi wasitoe kujionyesha machoni pa watu.Katika Matayo 6:1 ,Yesu akasema "Angalieni msitende wema machoni pa watu kusudi mtazamwe na wao"Tunapotoa sharti tu makini kwa tutadhamini nia zetu.Tumeitwa kujitoa kwa utukufu wa Mungu na kwa wema wa watu wake.Tunapotoa,wakristo sharti tutafute idhini ya Bwana na sio sifa na pongezi ya watu.
3. **Bwana Yesu Kristo anahitaji kila Mkristo afanye mazoea ya kutoa kwa ukarimu.**
   Katika Matayo 6:23, Yesu alisema " Unapopea maskini"Hapo Yesu afundisha kuhusu "Sadaka /Zaka"hiyo ni msaada ,upendo au sadaka za ukarimu kwa watu wenye mahitaji.Kila Mkristo ameitwa kutoa kwa wale wasiojiweza kuliko sisi .
4. **Yesu anakumbusha kila Mkristo kuwa kutoa ni kwa Baba wa Mbinguni aonaye mambo yote**.
   Katika Matayi 6:3-4 ,Yesu alisema, "Bali wewe utoapo---;na Baba yako aonaye sirini atakujazia"Tunatoa sio tu kwa kutimiza mahitaji ya kanisa bali kusudi ni kuonyesha Shukrani ama kumshukuru Mungu Baba wa Mbinguni.Kila Mkristo anakumbushwa kuwa jukumu letu la Msingi ni kutoa "Kama ambaye tunamtolea  Bwana Mungu Wetu".

5. **Biblia yatufunza kuwa kutoa kwa Mkristo ni tendo la Kuabudu.**
Mtume Paulo aweka hili bayana katika 1 Wakorintho 16:2 kwa kusema "Siku ya kwanza ya Juma,kila mtu kwenu na aweke akiba kwake"Kutoa kwetu na fungu la Juma ni sehemu ya tendo la kumwabudu Mungu kila mara katika sabato.Tunapotoa kila Jumapili tunamwabudu Mungu mwenye enzi kulingana na neno lake.Kila Mkristo sharti kulipa kipaumbele tendo la kutoa kama tendo la kumwabudu Mungu wala sio kutimiza bajeti ya Kanisa.

6. **Biblia Yatufunza kuwa kutoa kuwe dhabiti /kila mara na kwa mpangilio.**
Katika 1 Wakorintho 16:1-4 ,Paulo alisema kuwa kila mmoja aweke kiwango fulani kila mara ili kwamba michango isifanyike wanapokuja pamoja.Kutoa sharti kupangia kusiwe bila mpangilio bali kwa mwito wa hiari.Kwa hivyo ,tunapokutana isiwe tu tunazingatia hisia au hali zetu binafsi lakini iwe dhabiti katika kutoa.(1 Wakorintho 6:1-4).

Kwa kutamatisha,tunachokiona katika kanuni hizi na muhimu ni kweli kwamba sharti tutoe kwa sababu nzuri,toa kwa njia halali(mahala,muda na kiwango),na toa kwa kusudi la haki na kwa Mungu au Kanisa.Tunapochunguza utoaji wetu tukilinganisha na kanuni hizi za utoaji wa kikristo,tunabaini kuwa tuko chini ya uwezo na mwito wetu wa kutoa. Tunahitaji kuomba kwamba Kristo Yesu atupe neema ya kutoa inavyostahili ili tufurahie uaminifu na heshima kutoka kwa Mungu ambayo alitupa na anaendelea kutupa sisi vyote tulivyo navyo.

**Maswali ya Kutafakari.**

1. Iwapo ungejiweka kwenye mizani ,je,hali yako ni bora au mbaya ukilinganisha na mafundisho muhimu ya Mkristo kutoa ? Na kwa nini?
2. Je,ni vipi mafundisho ya Juma hili ya kutoa yamekusaidia na kukuhamasisha /kukuhimiza kuwa mtoaji mwaminifu?

**JUMA LA TATU.**

**MISINGI YA UTOAJI WA KIKRISTO**

*Vifungu vya Biblia:Zaburi 8:1,Luka 12:35,2 Wakorintho 8:1-15 na 2 Wakorintho 9:1-15.*

Ili tuwe Wakili waaminifu ,ni sharti tuwe na motisha iliyo sawa katika kutoa kwetu.Isitoshe kuelewa njia mbalimbali au badala za kutoa itatuandaa sisi katika kutoa kwetu kwa furaha kama Wakristo.

**1. Motisha ya Kutoa.**

Kwa kuwa Wakristo kila mara katika historia ya Ukristo hujitoa kwa nia nzuri kwa kazi ya kanisa,sisi pia tunashuhudia Wakristo ambao hutoa kwa nia mbaya Hii ni kwa sababu ya mafundisho mabaya na kutoelewa msingi wa kibibilia kuhusu kutoa.

**A Nia mbaya za Wakristo kutoa**

Ili kuelewa nia nzuri ya kutoa,hebu mwanzo tuangalie nia mbovu za kutoa.

1. Kutoa kwa minajili ya kutajirisha au kumsaidia Mungu .Mungu tayari ana kila kitu (Zaburi 50:12)

2. Kutoa bila kujijali sisi binafsi,familia na majukumu mengine tuliyo nayo.Katika hekima zake,Mungu huturuhusu kusalia na asilimia 90%.Toa kulingana na uwezo wako.

3. Kutoa ili kupokelewa na kukubalika.Bali tutoe kwa sababu tumepokea na kukubalika.Kanisa la Makedonia lilijitoa hata katika hali ya umaskini(2 Wakorintho 8:1, 2Wakorintho 8:9)

4. Kutoa ili kuwafurahisha au kuwavutia wengine.Bwana Yesu Kristo atuonya na kutuhadhari dhidi ya kujionyesha wenye haki mbele ya watu.(Matayo 6:1)Twafaa kutoa kwa utukufu wa Bwana Mungu Pekee.

**B. Nia nzuri za utoaji wa Kikristo.**

Zifuatazo ni nia nzuri za kutoa.

1. Lazima iwe kwa misingi ya ushawishi kuwa twampa Mungu kilicho chake kwa kuwa Mungu ndiye mwenye vitu vyote (1 Wakorintho 4:7).

2. Kutoa kwetu lazima tuhimizwe/kutiwa moyo na upendo ,wala si mambo mengine ya kujitakia.(2Wakorintho 8:8 na 9:7)

3. Twatoa kama furaha na Shukrani kuitikia baraka ambazo Mungu ametupa kwa ukarimu.Ndio maana twafanya tendo mazoea la kutoa wakati wa Kuabudu na kama ibada ( 1 Wakorintho 8:12).

4. Toa kulingana na baraka ambazo Mungu ametupatia (1 Wakorintho 16:2)wala si kwa vile tusivyo navyo( 1 Wakorintho 8:12).

5. Toa kwa kupenda na kwa iyari bila kulazimishwa 2 Wakorintho 9:7 yasema “Kila mmoja lazima afanye/atende kama alivyokusudia moyoni mwakr, bila kulazimishwa”

6. Twafaa kutoa kama kwamba tumetunukiwa kuonyesha Shukrani kwa yale Mungu tayari ametupa sisi,wala si kwa misingi wa yale Mungu anaenda kutenda!.

**2. Njia mbalimbali za kutoa.**

Hapa kuna aina mbili ya zaka ambazo wakristo wanastahili wakristo wanahitaji kutoa.

a. Matoleo ya kila mara .Hii yajumuisha fungu la kumi kwa kazi ya kanisa na wafanyikazi (Hesabu 18,Luka 10:1-9,Wagalitia 6:6 Wafilipi 4:14-19)

,

b. Matoleo maalum :yajumuisha.(i) Kutoa kwa ukarimu kwa maskini na wanaohitaji kama vile Yesu alituita sisi tuwe na uzoefu wa kutenda /kufanya (Matayo 6:2-3).(ii)Kutoa kwa miradi ya Kanisa kama vile ujenzi wa hekalu.2Wafalme 12:14-16,Mambo ya Nyakati 29:1-17,Matayo 17:24-27) na
(iii) Kujitolea kwa hiyari kutoa Sadaka kwa shuguli maalum kama vile shukrani kwa baraka maalum.

**3. Yesu mwenyewe kajitoa kuwa mfano kwetu sisi kujitoa.**

Msingi wa kweli kwa Wakristo kutoa ni kufuata mfano wa Kristo kujitoa kama mfano kwetu kwa 2 Wakorintho 8:9 ambapo Paulo aliandika “Kwenu nyinyi kutambua/kujua neema ya mwokozi wetu Yesu Kristo ya kuwa ingawa alikuwa tajiri,laikini kwa ajili yetu akawa maskini kwa kupitia umaskini wake tufanyike tajiri” Fungu la kumi ndiyo mwanzo,laikini malengo yetu ni kujitolea vikamikifu wenyewe ,sio sehemu tu na mali yetu.Tusiwe twauliza , “Ni kwa asilimia ndogo kiasii gani yakubalika kwangu mimi kutoa”,lakini tujiulize, “Ni kutoa kwa kiwango gani italinganishwa na gharama ya kujitoa kwa mwokozi kwa ajili yangu”

**Maswali Tafakari.**

1. Ni mara ngapi umefahamu nia zako za kutoa?
   Eleza jinsi somo/funzo hili limekufundisha kuwa makini unapotoa.
2. Masomo/mafunzo gani umepata katika Juma hili juu ya mafunzo ya uwakili?

**JUMA LA 4.**

**FAIDA ZA UWAKILI UAMINIFU.**

Vifungo Malaki 3:7-18,Zaburi 31:1,2 Wakorintho 9:6-15 na Wafilipi 4:10-20.

**I.Faida Jumlishi za uwakili mzuri wa Kikristo**.

a. Mafundisho ya fungu la kumi ni nzuri na wa haki kwa maskini na matajiri kwa vile ni sambamba/kulingana na uwezo wa mtu.

b. Inamfanya anayetoa kuwa na Baraka tele tele. (Malaki 3:10)

c. Inatoa rasilmali ya kutosha kwa kanisa na kwa kazi ya ufalme .

d. Inawasaidia wasiojiweza na maskini kwa sababu kanisa lawafikia.

e. Inalipunguzia kanisa wasiwasi na mzigo wa rasilmali chache ili kuweza kuzingatia maswala ya kiroho.

**II. Faida za uwakili mwema wa kutoa kwa uaminifu.**

Hapa Tutaangazia faida tatu za uaminifu wa uwakili wa fedha.

**1. Faida kwa wakili-Wewe na Mimi.**

a. Inakuwezesha kumuabudu Mungu wa kweli kwa njia nzuri. Uwakili mzuri unafanya fedha kuwa chombo muhimu cha kumuabudu Mungu na sio sanamu ya Kuabudu kama vile walimwengu wanavyofanya.Kwa hivyo inaweka fedha. mahali pake sawa kama chombo cha kumuabudu Munngu na kujenga ufalme wa Mungu.

b. Wakili mwaminifu huvuna thawabu nyingi.Mungu anaweza kumbariki mtu anayetoa kwa uaminifu hapa duniani Luka 6:38.Mariko 10:28-30,Matayo 6:33,Wafilipi 4:18-19 na Muamini atarithi raha ya Baba yetu juu mbinguni(”Mfano wa Ufalme”)katika Malaki 3:10 .Mungu anaahidi kuwapa Baraka tele

“Leteni zaka kamili ghalani ili kiwemo chakula katika nyumba yangu.Mukanijaribu kwa njia hiyo,asema Bwana wa Majeshi  mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kumwagieni Baraka ,hata isiwepo nafasi ya kutosha au la”Mungu  anaweza amua kutubariki kifedha au kutupa baraka nyingine za kiroho.Tunapomtolea Mungu yeye ana uwezo zaidi wa kutuzidishia yote tunayohitaji. Mwenyezi Mungu atatimiza mahitaji yetu binafsi tunapotoa kwa ukarimu.Kwa hivyo tunaposoma Maneno ya mtume Paulo katika waraka  wa Pili  wa Wakorintho 9:8“Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi ill nyinyi mkiwa na uwingi kwa kila kitu kila wakati siku zote mpate kuzidi sana katika kila tendo jema”.Hakuna hata mmoja awe na kidogo au kingi atakuwa maskini zaidi kwa sababu walimtolea  Mungu. Kwa kutamatisha,wanaopokea matoleo yetu watatuombea kwa upendoi mkuu kwa Jina au kumwomba Mungu awabariki wote waliosababisha wabarikiwe.

c. Uwakili mzuri unazababisha mungu kutuamini na huduma kubwa zaidi.Tunapozidi kuwa mawakili waaminifu Mungu antuamini na vitu vyake  ambayo hubadilika na kutupa nafasi nyingi za kuhudumu katika ufalme wake.Kwa ufupi, mawakili waaminifu humfanya Mungu kutuamini hata zaidi na nafasi nyingi za huduma.Hivyo basi katika Luka 16:9-11,Yesu anasema—Aliye mwaminifu katika lililo ndogo si huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia.

**2. Faida kwa Wengine.**

Uwakili mzuri husababisha utimilifu wa mahitaji ya wengine na kuwafanya kumheshimu Mungu. Wanaopokea huja kumpenda na kumtii Mungu kupitia kwa ukarimu wetu tunaposoma Matendo ya Mtume 4:32-34. Paulo atuonyesha jinsi kutoa fedha zetu kwa uaminifu husababisha Shukrani kutoka kwa wale ambao wamebarikiwa kwa ukarimu wetu wa kikristo .Wakorintho wa Pili 9:11-13.

**3. Faida kwa kanisa la Mungu.**

Uwakili mzuri hauleti Baraka tu kwetu sisi na wengine bali muhimu zaidi kwa kanisa la Mungu na kazi ya Mungu katika ulimwengu. Kupitia kutoa kwetu kwa uaminifu,tunadhibitisha kwamba Mungu ndiye mmiliki na kukubali kufinyangwa na mwenyezi Mungu kuwa dhabihu ya kutumika kwa madhamini /minajili yake.

Jinsi ilivyofanyika kwa Bwana Yesu ambaye alifanyika sadaka takatifu ya mwanakondooo kama mfano kwetu, kujitoa kwa uaminifu inaturuhusu sisi kuwa na mtindo huo wa kutoa sadaka ili kutumika kwa utukufu wa Mungu na kanisa lake.Hii yaeleza kwa nini Mungu anawapenda wanaotoa kwa furaha.Kinyume cha haya ni ukweli usiopingika ya kwamba Wakristo na kanisa ambalo hukataa kutoa kwa Mungu na wasiojiweza hukosa kumheshimu Mungu na Injili yake ya upendo wake na ukumbozi wa ulimwengu.

**iii. Tamati.**

Uwakili wa kuaminika huleta faida tele kwa yule anayetoa na anayepokea na malengo ya mwenyezi Mungu duniani.Faida hizo zilizotajwa hapo juu awali zikuhamasishe wewe kuwa wakili mwaminifu kwa mali ya Mungu ambayo amekupa.Kumbuka kwamba kwa kila tendo la kutoa tunatimiza dua katika sala ya Bwana, “Ufalme wako uje”

**Maswali ya Kutafakari.**

1. Je, faida za kutoa ambazo zimeorodheshwa hapa zaathiri vipi uwakili wako binafsi?
2. Ukweli gani mpya au za uhakika umejifunza kutokana na mafundisho ya uwakili wa jumaa hili?

**Diocesan Website**

www.ackkitalediocese.org

*Kukumbatia mambo mapya*
*Mungu anatenda*

Isaya 43:19-20